07

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR

# TOLEO LA TAKWIMU ZA AJALI NA MAKOSA YA BARABARANI KWA ZANZIBAR JULAI, MWAKA 2023

## OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

## Utangulizi

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ajali na makosa ya barabarani. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi makuu kumi na moja (11).


## Lengo

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabarani za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera, na watoa maamuzi.

## Ajali za Barabarani

Jumla ya ajali 24 zimeripotiwa mwezi wa Julai, 2023. Wilaya ya Micheweni imeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni tano (5) ikilinganishwa na wilaya nyengine.


**Kielelezo 1.1: Idadi ya Ajali za Barabarani Kwa Wilaya, Julai 2023**




Idadi ya Ajali za barabarani zilizotokea kwa mwezi Julai , 2023 zimeongezeka kutoka ajali 12 kwa mwezi wa Juni hadi ajali 24 kwa mwezi wa Julai 2023.

Kwa mwezi wa Julai 2023, wilaya ya Micheweni imeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni tano (5) ikilinganishwa na Mwezi wa Juni ambapo Magharibi ‘B’ na Kati ziliripotiwa kutokea ajali nyingi (4) kwa kila wilaya.


**Kielelezo 1.2: Mlinganisho wa Ajali za Barabarani kwa Mwezi wa Juni 2023 na Julai 2023**



Idadi ya Ajali za barabarani kwa mwaka uliopita zimeongezeka kutoka ajali 14 kwa mwezi wa Julai 2022 hadi ajali 24 kwa mwezi wa Julai 2023.


Kwa mwezi wa Julai, 2023, wilaya ya Micheweni imeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni tano (5) ikilinganishwa na Mwezi wa Julai 2022 ambapo wilaya ya Kaskazini "B" iliripotiwa kuwa na ajali nyingi (3).

**Kielelezo 1.3: Mlinganisho wa Ajali za Barabarani Kwa Mwezi wa Julai 2022 na Julai 2023**





Jumla ya waathirika 51 wameripotiwa mwezi wa Julai, 2023, ambapo waathirika 47 walikuwa wanaume na waathirika wanne (4) alikuwa wanawake. Wilaya ya Magharibi "A" imeripotiwa kuwa na waathirika wengi ambao ni 15 sawa na asilimia 29.4 ikilinganishwa na wilaya nyengine.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Waathirika wa Ajali za Barabarani, Julai 2023**





Waathirika waliofariki kwa mwezi Julai wameongezeka kwa asilimia 60.0 kutoka waathirika waliofariki 10 kwa mwezi wa Juni 2023 hadi waathirika waliofariki 16 kwa mwezi wa Julai 2023

**Kielelezo 1.5: Mlinganisho wa Waathirika Waliofariki kwa Mwezi wa Juni 2023 na Julai 2023**




Waathirika waliojeruhiwa kwa mwezi uliopita wameongezeka kutoka waathirika waliojeruhiwa 15 kwa mwezi wa Juni 2023, hadi waathirika 35 waliojeruhiwa mwezi wa Julai, 2023.

**Kielelezo 1.6: Mlinganisho wa Waathirika Waliojeruhiwa kwa Mwezi wa Juni 2023 na Julai 2023**





Waathirika Waliofariki kwa mwaka uliopita wameongezeka, aidha kwa mwezi wa Julai 2022 walikuwa waathirika 12 waliofariki ikilinganishwa na mwezi wa Julai, 2023 walikuwa waathirika 16 waliofariki.

**Kielelezo 1.7: Mlinganisho wa Waathirika Waliofariki kwa Mwezi wa Julai 2022 na Julai 2023**





Waathirika waliojeruhiwa kwa mwaka uliopita wameongezeka ambapo Julai 2022 walikuwa waathirika waliojeruhiwa ni 3 wakati kwa mwezi wa Julai, 2023 walikuwa waathirika 35 waliojeruhiwa.

**Kielelezo 1.8: Mlinganisho wa Waathirika Waliojeruhiwa kwa Mwezi wa Julai 2022 na Julai 2023**




Waathirika wengi inaonekana ni Wapanda baskeli na pikipiki. Miongoni mwa waathirika wa ajali za barabarani (waliojeruhiwa na waliofariki), Wapanda baskeli ni 16, Waendao kwa miguu 15, Abiria ni 15 na madereva walikuwa watano(5).

**Kielelezo 1.9: Idadi na Aina ya Waathirika wa Ajali za barabarani, Julai 2023**





Kwa mwezi wa Julai 2023, ajali zaidi zilitokea muda wa saa 12:01 jioni - 3:00 usiku ambapo zimeripotiwa ajali sita (6).

**Kielelezo 1.10: Idadi ya Ajali na Muda Uliotokea, Julai 2023**




Jumla ya ajali 24 zilizoripotiwa mwezi wa Julai, 2023 ambapo ajali zote zilisababishwa na kuendesha gari kwa mwendo kasi. Mkoa wa Mjini Magharibi na Mkoa wa Kaskazini Pemba inaongoza kuwa na ajali nyingi (sita 6) kwa kila Mkoa.

**Kielelezo 1.11: Chanzo cha Ajali za Barabarani kwa Mkoa Julai 2023**




## Makosa ya Barabarani

Jumla ya makosa 3,338 yameripotiwa mwezi wa Julai, 2023, ambapo makosa 3,330 yameripotiwa kufanywa na wanaume na makosa nane (8) yameripotiwa kwa wanawake.

Wilaya ya Kati ina idadi kubwa ya makosa ya barabarani (makosa 752) sawa na asilimia 22.5 ya makosa yote yaliyoripotiwa. Wilaya ya Micheweni ina idadi ndogo ya makosa ya barabarani, makosa 43 sawa na asilimia 1.3 ya makosa yote yaliyoripotiwa.


**Kielelezo 2.0: Idadi ya Makosa ya Barabarani Kwa Wilaya, Julai 2023**




Kosa kuu lililoripotiwa kwa mwezi wa Julai, 2023 ni Kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (makosa 1,163 ) yakifuatia na Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia (makosa 854) na Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo (makosa 679 ) .

Orodha ya makosa haya matatu (3) ya barabarani kati ya yote tisa (9) yaliyoripotiwa yamechangia asilimia 80.8.


Kielelezo 2.1: Idadi na Aina ya Makosa ya Barabarani,Julai 2023



Idadi ya makosa kwa mwezi uliopita yameongezeka kwa asilimia 5.1 kutoka makosa 3,175 mwezi wa Juni 2023 hadi 3,338 mwezi wa Julai 2023.

Wilaya ya Kati iliongoza kuwa na idadi kubwa ya makosa ya barabarani kwa mwezi wa Juni 2023 (makosa 743) na Julai 2023 (Makosa 752).


**Kielelezo 2.2: Mlinganisho wa Idadi ya Makosa ya Barabarani Kwa Mwezi wa Juni 2023 na Julai 2023**




Idadi ya makosa ya barabarani kwa mwaka wa Julai, 2023 na Julai 2022 imeongezeka. Aidha, jumla ya makosa 3,338 yameripotiwa kwa mwezi wa Julai, 2023 ikilinganishwa na makosa1,442 yaliyoripotiwa mwezi wa Julai 2022.

Wilaya ya Kati imeongoza kwa makosa ya barabarani kwa mwezi wa Julai 2023 ikiwa na idadi ya makosa 752 ikilinganishwa na wilaya ya Mjini iliyoongoza kwa makosa 217 kwa mwezi wa Julai, 2022

**Kielelezo 2.3: Mlinganisho wa Idadi ya Makosa ya Barabarani kwa Mwezi wa Julai 2022 na Julai 2023**



## HITIMISHO

Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi makuu kumi na moja (11). Lengo la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabarani za ndani ya Zanzibar.

Jumla ya ajali 24 zimeripotiwa mwezi wa Julai, 2023. Wilaya Micheweni imeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni tano (5) ikilinganishwa na wilaya nyengine.
Mlinganisho wa idadi ya Ajali za barabarani zilizotokea kwa mwezi Julai, 2023 zimeongezeka kutoka ajali 12 kwa mwezi wa Juni hadi ajali 24 kwa mwezi wa Julai 2023.

Jumla ya makosa 3,338 yameripotiwa mwezi wa Julai, 2023, ambapo makosa 3,330 yameripotiwa kwa wanaume na makosa nane (8) yameripotiwa kwa wanawake. Wilaya ya Kati ina idadi kubwa ya makosa ya barabarani (makosa 752) sawa na asilimia 22.5 kati ya makosa tisa (9) yaliyoripotiwa. Kosa kuu lililoripotiwa kwa mwezi wa Julai, 2023 ni Kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (makosa 1,163 ).

## Kiambatanisho:

**Jadweli 3.0: Idadi na Asilimia ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Julai 2023**

| Wilaya | Idadi ya ajali | | Waliokufa | | | | Waliojeruhiwa | | | | Jumla | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Nambari | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia |
| Kaskazini 'A' | 2 | 8.3 | 3 | 0 | 3 | 18.8 | 1 | 0 | 1 | 2.9 | 4 | 0 | 4 | 7.8 |
| Kaskazini 'B' | 3 | 12.5 | 2 | 1 | 3 | 18.8 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 2 | 1 | 3 | 5.9 |
| Kati | 3 | 12.5 | 2 | 0 | 2 | 12.5 | 3 | 0 | 3 | 8.6 | 5 | 0 | 5 | 9.8 |
| Kusini | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| Mjini | 1 | 4.2 | 0 | 1 | 1 | 6.3 | 1 | 0 | 1 | 2.9 | 1 | 1 | 2 | 3.9 |
| Magharibi 'A' | 3 | 12.5 | 1 | 0 | 1 | 6.3 | 13 | 1 | 14 | 40.0 | 14 | 1 | 15 | 29.4 |
| Magharibi 'B' | 2 | 8.3 | 1 | 1 | 2 | 12.5 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 1 | 1 | 2 | 3.9 |
| Wete | 1 | 4.2 | 1 | 0 | 1 | 6.3 | 2 | 0 | 2 | 5.7 | 3 | 0 | 3 | 5.9 |
| Micheweni | 5 | 20.8 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 8 | 0 | 8 | 22.9 | 8 | 0 | 8 | 15.7 |
| Chake chake | 3 | 12.5 | 2 | 0 | 2 | 12.5 | 5 | 0 | 5 | 14.3 | 7 | 0 | 7 | 13.7 |
| Mkoani | 1 | 4.2 | 1 | 0 | 1 | 6.3 | 1 | 0 | 1 | 2.9 | 2 | 0 | 2 | 3.9 |
| **Zanzibar** | **24** | **100** | **13** | **3** | **16** | **100** | **34** | **1** | **35** | **100** | **47** | **4** | **51** | **100** |

## Jadweli 3.1: Idadi ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Julai 2023

| Wilaya | Idadi ya ajali | Dereva | | | | | | Abiria | | | | | | Wapanda baskeli na pikipiki | | | | | | Waendao kwa miguu | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | W liokufa | | | Waliojeruhiwa | | | W liokufa | | | Waliojeruhiwa | | | W liokufa | | | Waliojeruhiwa | | | W liokufa | | | Waliojeruhiwa | | |
| | | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T |
| Kaskazini 'A' | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 8 | 1 | 9 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 |
| Magharibi 'B' | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 4 |
| Chake chake | 3 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **24** | **0** | **0** | **0** | **5** | **0** | **5** | **1** | **1** | **2** | **12** | **1** | **13** | **6** | **0** | **6** | **10** | **0** | **10** | **6** | **2** | **8** | **7** | **0** | **7** |

## Jadweli 3.2: Mlinganisho wa Idadi ya Ajali Barabarani baina ya Mwezi wa Julai 2022 na Julai 2023

| Wilaya | Idadi ya ajali | | Waathirika | | | | Dereva | | | | Abiria | | | | Wapanda baskeli na Pikipiki | | | | Waendao kwa Miguu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | |
| | Julai - 22 | Julai - 23 | Julai - 22 | Julai - 23 | Julai - 22 | Julai - 23 | Julai - 22 | Julai - 23 | Julai - 22 | Julai - 23 | Julai - 22 | Julai - 23 | Julai - 22 | Julai - 23 | Julai - 22 | Julai - 23 | Julai - 22 | Julai - 23 | Julai - 22 | Julai - 23 | Julai - 22 | Julai - 23 |
| Kaskazini 'A' | 2 | 2 | 0 | 1 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Kaskazini 'B' | 3 | 3 | 0 | 0 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kati | 2 | 3 | 0 | 3 | 2 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 |
| Kusini | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mjini | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 2 | 3 | 0 | 14 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 | 0 | 1 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 |
| Magharibi 'B' | 1 | 2 | 2 | 0 | 1 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Wete | 1 | 1 | 1 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 1 | 5 | 0 | 8 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 |
| Chake chake | 1 | 3 | 0 | 5 | 1 | 2 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Mkoani | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| **Zanzibar** | **14** | **24** | **3** | **35** | **12** | **16** | **1** | **5** | **0** | **0** | **1** | **13** | **2** | **2** | **2** | **10** | **5** | **6** | **0** | **7** | **4** | **8** |

## Jadweli 3.3: Mlinganisho wa Idadi ya Ajali Barabarani baina ya Mwezi Juni 2023 na Julai 2023

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Walioathirika | | | | Dereva | | | | Abiria | | | | Wapanda baskeli na pikipiki | | | | Waendao kwa Miguu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | |
| | Juni 2023 | Julai 2023 | Juni 2023 | Julai 2023 | Juni 2023 | Julai 2023 | Juni 2023 | Julai 2023 | Juni 2023 | Julai 2023 | Juni 2023 | Julai 2023 | Juni 2023 | Julai 2023 | Juni 2023 | Julai 2023 | Juni 2023 | Julai 2023 | Juni 2023 | Julai 2023 | Juni 2023 | Julai 2023 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kati | 4 | 3 | 0 | 3 | 4 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 |
| Kusini | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mjini | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 1 | 3 | 3 | 14 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 9 | 1 | 1 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 4 | 2 | 9 | 0 | 4 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Wete | 2 | 1 | 3 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 5 | 0 | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 0 | 3 | 0 | 5 | 0 | 2 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Mkoani | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| **Zanzibar** | **12** | **24** | **15** | **35** | **10** | **16** | **0** | **5** | **0** | **0** | **9** | **13** | **2** | **2** | **6** | **10** | **6** | **6** | **0** | **7** | **2** | **8** |

### Jadweli 3.4: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa Kwa Wilaya na Jinsi, Julai 2023

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | | Uendeshaji hatari | | | Ubovu wa vipando | | | Kuendesha chombo cha motobila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 25 | 0 | 25 | 15 | 0 | 15 | 80 | 0 | 80 | 130 | 0 | 130 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 10 | 0 | 10 | 0 | 0 | 0 | 105 | 0 | 105 | 100 | 0 | 100 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 167 | 0 | 167 | 27 | 0 | 27 | 170 | 3 | 173 | 152 | 0 | 152 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 4 | 0 | 4 | 10 | 0 | 10 | 53 | 0 | 53 | 40 | 0 | 40 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 31 | 0 | 31 | 174 | 0 | 174 | 28 | 0 | 28 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 19 | 0 | 19 | 141 | 0 | 141 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 44 | 0 | 44 | 192 | 0 | 192 | 12 | 0 | 12 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 2 | 0 | 2 | 12 | 0 | 12 | 35 | 0 | 35 | 12 | 0 | 12 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 | 0 | 11 | 15 | 0 | 15 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 10 | 5 | 2 | 7 | 20 | 0 | 20 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 15 | 3 | 18 | 5 | 0 | 5 | 29 | 0 | 29 |
| **Zanzibar** | **0** | **0** | **0** | **12** | **0** | **12** | **208** | **0** | **208** | **164** | **3** | **167** | **849** | **5** | **854** | **679** | **0** | **679** |

**Inaendelea… Jadweli 3.4: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa kwa Wilaya na Jinsi, Julai 2023**

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa utingo na dereva kwa gari za abiria | | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 5 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 20 | 0 | 20 | 120 | 0 | 120 | 0 | 0 | 0 | 395 | 0 | 395 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 20 | 0 | 20 | 135 | 0 | 135 | 0 | 0 | 0 | 373 | 0 | 373 |
| Kati | 6 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 23 | 0 | 23 | 201 | 0 | 201 | 0 | 0 | 0 | 749 | 3 | 752 |
| Kusini | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 15 | 0 | 15 | 105 | 0 | 105 | 6 | 0 | 6 | 238 | 0 | 238 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 27 | 0 | 27 | 290 | 0 | 290 | 0 | 0 | 0 | 550 | 0 | 550 |
| Magharibi 'A' | 36 | 0 | 36 | 0 | 0 | 0 | 14 | 0 | 14 | 104 | 0 | 104 | 0 | 0 | 0 | 314 | 0 | 314 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 10 | 149 | 0 | 149 | 0 | 0 | 0 | 407 | 0 | 407 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 | 0 | 9 | 17 | 0 | 17 | 0 | 0 | 0 | 90 | 0 | 90 |
| Micheweni | 16 | 0 | 16 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 43 | 0 | 43 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 29 | 0 | 29 | 21 | 0 | 21 | 0 | 0 | 0 | 85 | 2 | 87 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 17 | 0 | 17 | 20 | 0 | 20 | 0 | 0 | 0 | 86 | 3 | 89 |
| **Zanzibar** | **65** | **0** | **65** | **0** | **0** | **0** | **184** | **0** | **184** | **1,163** | **0** | **1,163** | **6** | **0** | **6** | **3,330** | **8** | **3,338** |

Jadweli 3.5: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Julai, 2022 na Julai, 2023

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | Uendeshaji hatari | | Ubovu wa vipando | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | Kuzidisha idadi yaabiria na mizigo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Julai 2022 | Julai 2023 | Julai 2022 | Julai 2023 | Julai 2022 | Julai 2023 | Julai 2022 | Julai 2023 | Julai 2022 | Julai 2023 | Julai 2022 | Julai 2023 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 25 | 4 | 15 | 31 | 80 | 69 | 130 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 34 | 3 | 0 | 10 | 3 | 0 | 4 | 105 | 47 | 100 |
| Kati | 0 | 0 | 1 | 3 | 31 | 167 | 8 | 27 | 21 | 173 | 59 | 152 |
| Kusini | 0 | 0 | 2 | 3 | 0 | 4 | 0 | 10 | 1 | 53 | 8 | 40 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 32 | 31 | 67 | 174 | 36 | 28 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 44 | 0 | 63 | 19 | 14 | 141 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 77 | 44 | 55 | 192 | 19 | 12 |
| Wete | 0 | 0 | 1 | 3 | 4 | 2 | 8 | 12 | 15 | 35 | 10 | 12 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 | 0 | 22 | 11 | 17 | 15 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8 | 10 | 58 | 7 | 19 | 20 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 15 | 18 | 20 | 5 | 29 | 29 |
| **Zanzibar** | **0** | **0** | **38** | **12** | **39** | **208** | **211** | **167** | **357** | **854** | **327** | **679** |

## Inaendelea… Jadweli 3.5: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Julai, 2022 na Julai, 2023

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa Utingo na dereva kwa gari za abiria | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Julai 2022 | Julai 2023 | Julai 2022 | Julai 2023 | Julai 2022 | Julai 2023 | Julai 2022 | Julai 2023 | Julai 2022 | Julai 2023 | Julai 2022 | Julai 2023 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 5 | 0 | 0 | 7 | 20 | 19 | 120 | 0 | 0 | 134 | 395 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 20 | 20 | 63 | 135 | 0 | 0 | 171 | 373 |
| Kati | 7 | 6 | 0 | 0 | 34 | 23 | 15 | 201 | 0 | 0 | 176 | 752 |
| Kusini | 0 | 2 | 0 | 0 | 4 | 15 | 6 | 105 | 0 | 6 | 21 | 238 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 22 | 27 | 60 | 290 | 0 | 0 | 217 | 550 |
| Magharibi 'A' | 0 | 36 | 0 | 0 | 12 | 14 | 16 | 104 | 0 | 0 | 149 | 314 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 14 | 10 | 28 | 149 | 0 | 0 | 193 | 407 |
| Wete | 1 | 0 | 0 | 0 | 4 | 9 | 30 | 17 | 0 | 0 | 73 | 90 |
| Micheweni | 0 | 16 | 0 | 0 | 3 | 0 | 9 | 1 | 0 | 0 | 63 | 43 |
| Chake chake | 9 | 0 | 0 | 0 | 22 | 29 | 41 | 21 | 0 | 0 | 157 | 87 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 | 17 | 13 | 20 | 0 | 0 | 88 | 89 |
| **Zanzibar** | **17** | **65** | **0** | **0** | **153** | **184** | **300** | **1,163** | **0** | **6** | **1,442** | **3,338** |

**Jadweli 3.6: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Juni 2023 na Julai 2023**

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | Uendeshaji hatari | | Ubovu wa vipando | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Juni 2023 | Julai 2023 | Juni 2023 | Julai 2023 | Juni 2023 | Julai 2023 | Juni 2023 | Julai 2023 | Juni 2023 | Julai 2023 | Juni 2023 | Julai 2023 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 5 | 0 | 5 | 25 | 17 | 15 | 58 | 80 | 224 | 130 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 3 | 3 | 2 | 10 | 4 | 0 | 32 | 105 | 108 | 100 |
| Kati | 0 | 0 | 2 | 3 | 113 | 167 | 4 | 27 | 238 | 173 | 212 | 152 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 4 | 4 | 10 | 0 | 53 | 31 | 40 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 39 | 31 | 110 | 174 | 40 | 28 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 69 | 0 | 94 | 19 | 30 | 141 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 114 | 44 | 77 | 192 | 16 | 12 |
| Wete | 0 | 0 | 10 | 3 | 1 | 2 | 15 | 12 | 56 | 35 | 7 | 12 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 23 | 11 | 3 | 15 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 20 | 10 | 12 | 7 | 40 | 20 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 18 | 18 | 8 | 5 | 9 | 29 |
| **Zanzibar** | **0** | **0** | **20** | **12** | **121** | **208** | **306** | **167** | **708** | **854** | **720** | **679** |


**Inaendelea… Jadweli 3.6: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Juni na Julai 2023**

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa Utingo na dereva kwa gari za abiria | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Juni 2023 | Julai 2023 | Juni 2023 | Julai 2023 | Juni 2023 | Julai 2023 | Juni 2023 | Julai 2023 | Juni 2023 | Julai 2023 | Juni 2023 | Julai 2023 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 5 | 0 | 0 | 15 | 20 | 225 | 120 | 3 | 0 | 552 | 395 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 20 | 146 | 135 | 2 | 0 | 300 | 373 |
| Kati | 7 | 6 | 0 | 0 | 76 | 23 | 91 | 201 | 0 | 0 | 743 | 752 |
| Kusini | 0 | 2 | 0 | 0 | 25 | 15 | 124 | 105 | 3 | 6 | 187 | 238 |
| Mjini | 0 | 0 | 57 | 0 | 0 | 27 | 115 | 290 | 0 | 0 | 361 | 550 |
| Magharibi 'A' | 0 | 36 | 0 | 0 | 42 | 14 | 113 | 104 | 0 | 0 | 348 | 314 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 31 | 10 | 60 | 149 | 0 | 0 | 298 | 407 |
| Wete | 11 | 0 | 0 | 0 | 7 | 9 | 32 | 17 | 0 | 0 | 139 | 90 |
| Micheweni | 0 | 16 | 0 | 0 | 2 | 0 | 4 | 1 | 0 | 0 | 34 | 43 |
| Chake chake | 5 | 0 | 0 | 0 | 30 | 29 | 30 | 21 | 0 | 0 | 137 | 87 |
| Mkoani | 8 | 0 | 0 | 0 | 20 | 17 | 13 | 20 | 0 | 0 | 76 | 89 |
| **Zanzibar** | **31** | **65** | **57** | **0** | **251** | **184** | **953** | **1,163** | **8** | **6** | **3,175** | **3,338** |


**Jadweli 3.7 Tozo zilizolipwa Mahakamani Kwa Wilaya na Idadi ya kesi, Julai 2023**

| Wilaya | Idadi ya kesi | Tozo(Shilingi) |
|---|---|---|
| Kaskazini 'A' | 389 | 15,735,875 |
| Kaskazini 'B' | 379 | 9,735,875 |
| Kati | 220 | 14,322,000 |
| Kusini | 235 | 2,323,800 |
| Mjini | 511 | 39,267,250 |
| Magharibi 'A' | 310 | 13,819,000 |
| Magharibi 'B' | 375 | 27,716,000 |
| Wete | 88 | 3,136,300 |
| Micheweni | 41 | 853,000 |
| Chake chake | 75 | 2,312,500 |
| Mkoani | 80 | 1,827,500 |
| **Zanzibar** | **2,703** | **131,049,100** |

**Kielelezo1: Ajali za Barabarani za Barabarani Zilizoripoti kwa Wilaya, Julai 2023**



**Kielelezo 2:Vifo na Majeruhi Wanaotokana na Ajali za Barabarani kwa Wilaya, Julai 2023**



## Zingatia Maelezo

Ajali ya barabarani inahusu ajali yeyote inayohusisha angalau gari moja barabarani, inayotokea barabarani kwa mzunguko wa umma na angalau mtu mmoja amekufa au amejeruhiwa. Kutokana na Sheria ya Adhabu nambari.6/2004 kuondoa Amri ya Adhabu, sura ya 13 ya sheria ya Zanzibar (Penal Act no. 6/2004 Act to repeal the Penal Decree, chapter 13 of the law of Zanzibar).

Kifo imefafanua iwapo kama watu wamepata ajali na kufa papo hapo au ndani ya mwaka mmoja na siku moja (366) baada ya ajali.

Watu waliojeruhiwa na waathirika kwa ajali waliopatwa na mshtuko wanaohitaji matibabu ya Hospitali au bila hospitali.

Njia kimsingi ina maana ya usafiri. Hio humpa binadamu kufikia maeneo tofauti. Watu wengi hutumia njia tofauti za usafiri. Baadhi yao hutumia gari, baiskeli na kwa miguu.

Kosa ni uhalifu ambao huvunja sheria fulani na kuwepo adhabu maalum. Ajali za barabarani husababishwa na makosa mbalimbali ya binadamu. Makosa mengi ambayo yanaonekana kuwa ni madogo lakini athari yake inakuwa kubwa. Matokeo yake watu hupata ulemavu au kufa.

**KWA UFAFANUZI ZAIDI TAFADHALI WASILIANA NA:**

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua, 2321, MMP, Zanzibar
Simu: +255242231869
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237
Barua pepe:cidphqznz@gmail.com
Nukushi: 024223136